JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**

# TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

---

*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023)*

**7 MEI, 2025**

## YALIYOMO

*Ukurasa*

**ORODHA YA MAJEDWALI** .......... ii
**ORODHA YA CHATI** .......... iii
**SEHEMU YA KWANZA** .......... 1
1.0 **UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Maelezo ya Jumla .......... 1
1.2 Muundo wa Taarifa .......... 1
1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati .......... 2
1.3.1 Msingi .......... 2
1.3.2 Mbinu na Njia Zilizotumika .......... 3
1.3.3 Wigo wa Kazi .......... 4
1.4 Majumuisho ya Sehemu .......... 5
**SEHEMU YA PILI** .......... 6
2.0 **MAELEZO YA JUMLA** .......... 6
2.1 Maelezo ya Jumla .......... 6
2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji .......... 6
2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati .......... 7
2.2.2 Ukusaji wa Maduhuli .......... 10
2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo .......... 14
2.2.4 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa .......... 15
2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti .......... 16
2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi .......... 18
2.3.1 Makadirio ya Mapato .......... 19
2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo .......... 23
2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida .......... 25
2.4 Majumuisho ya Sehemu ya Pili .......... 26
**SEHEMU YA TATU** .......... 28
**3.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO** .......... 28
3.1 Maelezo ya Jumla .......... 28
3.2 Maoni .......... 28
3.3 Ushauri .......... 29
3.4 Hitimisho .......... 30
**KIAMBATISHO NA 1** .......... 33
**KIAMBATISHO NA 2** .......... 39

## ORODHA YA MAJEDWALI

*Ukurasa*

**Jedwali Na. 1** : Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/20255 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ................... 10

**Jedwali Na. 2 :** Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 .... 17

**Jedwali Na. 3** : Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026 ........................................................................ 19

**Jedwali Na. 4 :** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026 ........................................................................ 24

# ORODHA YA CHATI

***Ukurasa***

**Chati Na. 1 :** Asilimia ya Jumla ya Malengo ya Wizara........................................ 11

**Chati Na. 2:** Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 …………….. 18

**Chati Na. 3 :** Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2024/2025 na mwaka 2025/2026........................................................................ 20

**Chati Na. 4:** Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026 ........................................................................ 25

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (**Fungu 96**) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Taarifa hii ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 11 hadi 27 Machi, 2025 kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi kwa Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa urahisi wa Bunge kufuatilia maudhui ya taarifa inayowasilishwa, sehemu hii inabainisha mtiririko wa Taarifa kwa kueleza muundo wake. Lengo ni kuonesha namna vigezo vya Taarifa za Kamati vilivyozingatiwa na kuonesha uhalali wa uchambuzi, maoni na ushauri unaotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulithibitishia Bunge kuwa, Muundo wa Taarifa hii umezingatia Masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge, kuhusu muundo wa Tarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii

imegawanyika katika sehumu kuu tatu kwa mujibu wa masharti ya Kanuni za Bunge. Sehemu hizo ni:

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii.
(ii) Sehemu ya **Pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii Mwaka wa fedha 2024/2025 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;
(iii) Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati

### 1.3.1 Msingi

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Taarifa ya Kamati kuhusu Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Nyongeza ya Nane chini ya Kanuni ya 137, imeweka masharti yanayofafanua jukumu la Kamati hii kufanyia kazi Makadirio ya Mapato na Matumizi, Fungu 96.

**Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 6 (7) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kifungu

cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Aidha, Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kabla kuwasilishwa Bungeni leo. Naomba kulihakikishia Bunge hili kuwa masharti hayo yalitimizwa,

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii imewekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.3.2 Mbinu na Njia Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** kubainisha njia iliyotumiwa na Kamati kufanyia kazi hoja hii ni masharti ya Kanuni ya 142 (a) ya Kanuni za Bunge. Madhumuni yake ni kuiwezesha Taarifa kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ilikupata maoni na ushauri wake.

**Mheshimiwa Spika,** mbinu za uchambuzi zilijumuisha kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na hali halisi. Yote hayo yamewezesha kupatikana kwa taarifa hii ambayo

inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 1.3.3 Wigo wa Kazi

**Mheshimiwa Spika,** kama inavyofahamika, lengo la Taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya kina na yenye ushahidi kuhusu makadirio ya matumizi na mapato yaliyowasilishwa na Mtoa hoja. Madhumuni yake ni kuongoza mjadala, kuonesha uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa na mahitaji halisi ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, Taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa Bunge lilipopitisha bajeti ya wizara hii. Eneo lingine la maudhui ya Taarifa hii linagusa makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na matarajio ya wananchi na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** mambo yote nje ya maeneo niliyoyaeleza si sehemu ya taarifa hii. Sababu ya kufanya hivyo ni kuchunga masharti ya 71 (1) ya Kanuni za Bunge kuhusu mambo

yasiyoruhusiwa. Jumla ya yote, wigo huo ni muhimu kwa taratibu bora za Bunge kujadili hoja ya Wizara hii.

### 1.4 Majumuisho ya Sehemu

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Sehemu ya Kwanza imeanza kwa ombi la kuiwasilisha rasmi Taarifa hii katika majadiliano ya Bunge, kuonesha muundo wa Taarifa hii unavyozingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge na kubainisha msingi wa Kamati kufanyia kazi makadirio ya Wizara hii. Kanuni zilizojenga msingi huo ni Kanuni ya 137 inayoweka masharti katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge ambayo inaonesha majukumu ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** nyingine ni Kanuni ya 118 inayohusu masharti ya makadilirio haya kujadiliwa kwanza na Kamati kabla ya Bunge, Kamati kuweka mezani taarifa mapema asubuhi kama ilivyofanyika na Kamati kuwasilisha rasmi wakati wa majadiliano kama inavyofanyika sasa. Vilevile, Kanuni ya 142 inayotaka Taarifa yoyote ya Kamati kuwekwa katika sehemu kuu tatu ni msingi wa Taarifa hii.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO YA JUMLA

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge ndiyo inahusu maelezo kamili ya uchambuzi wa Kamati. Uchambuzi huo ulifanyika kwa kuzingatia utaratibu uliowekewa masharti chini ya Kanuni ya 117 ya Kanuni za Bunge. Kwa ujumla masharti hayo yanahusu kuwasilishwa kwa dondoo za makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali, Randama za Makadirio hayo, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na ulinganisho wa taarifa za utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha kwa kuzingatia makadirio kwa mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya kuzingatia hayo yanatolewa taarifa katika sehemu hii. Aidha uchambuzi uliofanyika unabainishwa wazi ili kuliwezesha Bunge kufanya uamuzi kwa misingi ya taarifa sahihi zilizofanyiwa uchambuzi. Kwa urahisi wa mtiririko na ufuatiliaji, sehemu hii itaanza na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 na kumalizia na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, imeweka sharti la kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha, kwa lengo la kuwezesha

ulinganisho. Utaratibu huo unazingatia umuhimu wa tathmini ya matumizi yaliyopita kwenye msingi wa upangaji wa bajeti mpya kwa uwajibikaji, ushahidi na uhalisia. Taarifa ya Kamati kuhusu eneo hili, inalenga kuliwezesha Bunge libaini utekelezaji wa malengo ya Wizara, changamoto zilizojitokeza, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha na matumizi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni hayo, sehemu hii inatoa matokeo ya uchambuzi wa mambo matano ambayo ni:-

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

(ii) Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli

(iv) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuwezesha fursa kwa Bunge na umma kufahamu kama Serikali inazingatia ushauri uliotolewa Bungeni katika kuboresha matumizi ya rasilimali za umma, sehemu hii ya Taarifa inatoa mrejesho mbele ya Bunge. Kwa kufanya hivyo, taarifa hii inapima dhamira ya Serikali katika kutekeleza mipango na miradi kwa ufanisi ili kuwa na kigezo cha uamuzi katika kupitisha makadirio haya.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake ni endelevu kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa ushauri uliofanyiwa kazi unahusu jukumu la Serikali kuimarisha uratibu na usimamizi wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kuwa Wizara iliingia makubaliano na Mkusanya Madeni *(debts collector) ambaye ni* Mchinga Auction Mart and Real Agency Company Limited, tarehe 12 Agosti, 2024 kwa ajili ya kukusanya madeni ya wadaiwa sugu.

**Mheshimiwa Spika,** wadaiwa hao ni wale waliowezeshwa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kabla ya kuingia katika ushirikiano na Taasisi za Fedha. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, kiasi kilichokuswanya ni **Shilingi 68,265,875** kati ya **Shilingi 363,789,395** zilizokuwa zinadaiwa. Mwendelezo wa hilo umeripotiwa kwamba, Wizara inaendelea kumsimamia Mkusanya Madeni ili akamilishe jukumu lake kulingana na mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na utekelezaji mzuri wa ushauri, upo ushauri ambao utahitaji kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Mathalan, ushauri kuhusu Serikali kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha Mkandarasi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa anamaliza kazi kwa wakati ili kuruhusu michezo iliyozuiliwa kuendelea katika Uwanja huo. Maelezo ya Serikali yalibainisha kwamba, Serikali inafuatilia kwa karibu ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufuatiliaji huo ipo changamoto inayosababisha uwanja huu kushindwa kukamilika kwa wakati. Changamoto hiyo inahusu Uwanja wa Benjamin Mkapa kuwa uwanja pekee ambao unakidhi vigezo vyote vya FIFA. Hali hiyo, inasababisha wadau kuendelea kufanyia michezo yao katika uwanja wakati wa ukarabati. Hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na Wizara yanahitaji msisitizo wa kibunge katika kulifanyia kazi suala hilo. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali inapaswa kuzingatia ipasavyo msisitizo kwamba, suala la mikakati madhubuti ya kuhakikisha Mkandarasi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa anamaliza kazi kwa wakati, linapaswa kuzingatiwa inavyostahili.

### 2.2.2 Ukusaji wa Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 39,689,676,000.** Hadi kufikia Mwezi Februari 2025 Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ilikuwa imekusanya **Shilingi 15,712,441,407.23** Sawa na **Asilimia 40** ya malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na 1

**Jedwali Na. 1: Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2024/20255 - Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | % YA LENGO | % YA # LENGO | % YA # MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| **WIZARA** | 1,430,003,000 | 538,285,083.00 | 38 | 4 | 3 |
| **TAASISI** | 38,259,673,000 | 15,174,156,324.23 | 40 | 96 | 97 |
| **JUMLA** | 39,689,676,000 | 15,712,441,407.23 | 40 | 100 | 100 |


**Chanzo:** Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026

**Chati Na. 1 : Asilimia ya Jumla ya Malengo ya Wizara**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Jedwali Na, 1 la Taarifa hii*

**Chati Na. 2: Asilimia ya Jumla ya Makusanyo ya Wizara**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Jedwali Na, 1 la Taarifa hii*

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali na Chati hizo zinaonesha kama ifuatavyo:

(i) Wakati wa kukadiria makusanyo, uwiano wa chanzo cha makusanyo ya wizara kwa lengo ulikuwa ni 4% na uwiano wa makusanyo ya Taasisi zilizochini ya Wizara ulikuwa ni 96%;

(ii) Wakati wa utekelezaji, uwiano wa makusanyo ya wizara kwa jumla ya makusanyo yote umekuwa 3% na uwiano wa Mkusanyo ya Taasisi za Wizara umekuwa 97%;

(iii) Mwenendo wa Jumla wa makusanyo hadi kufikia Mwezi Februari, 2025 ni 40% ambayo ni pungufu ya nusu ilhali kipindi cha utekelezaji kimevuka nusu mwaka;

(iv) Uwiano wa masanyo kwa lengo chini ya Wizara, umekuwa hafifu zaidi ya Taasisi zilizo chini ya wizara. Wakati Wizara imefikia 38% ya Lengo, Taasisi zimefikia 40% ya lengo.

(v) Kwa ujumla mwenendo wa makusanyo kwa baadhi ya taasisi ni hafufu zaidi. Mathalani Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) imekusanya **28.6**% ya lengo la makusanyo yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa matokeo hayo ya uchambuzi, ni wazi kuwa uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo ni mdogo.

Hali hii inaathiri utekelezaji wa bajeti kuu ya serikali kwa kuwa makusanyo hayo ni sehemu ya mapato iliyozingatiwa katika bajeti ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge hili linapaswa kufahamu sababu za mwenendo duni wa makusanyo kwa kuwa hali ilivyo ni ishara ya mojawapo kati ya mambo mawili: Kwanza ni uwezekano wa lengo kuwa limepangwa bila kuzingatia uhalisia au kuna changamoto iliyozuia ufikiaji wa lengo. Kamati ilipotaka kujua sababu ilibaini kuwa, kutokukamilika kwa baadhi ya miradi kulichangia pengo la ufikiaji wa lengo. Kwa mfano, kutokukamilika kwa Mradi wa Kiwanda cha Uchapaji ambao ulipangwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2023/2024 kumeikosesha TSN mapato yaliyolengwa.

**Mheshimiwa Spika**, sababu nyingine ni mabadiliko ya teknolojia yaliyoathiri baadhi ya vyanzo vya mapato. Miongoni mwa vyanzo vilivyoathiriwa na mabadiliko hayo ni mauzo ya magazeti kutokana na kushuka kwa biashara ya uchapishaji na kusambaza habari kwa njia ya magazeti kutokana na matumizi ya TEHAMA katika muundo mwingine wa habari.

**Mheshimiwa Spika,** hayo yote kwa pamoja ni uzoefu unaostahili kuzingatiwa katika mwaka wa fedha 2025/2026. Mabadiliko ya Teknolojia ni jambo lisiloepukika kwa sekta ya habari, sekta ya Sanaa na michezo na sekta ya utamaduni zinahitaji kuendeshwa kulingana na mabadiliko ya mara kwa

mara ya teknolojia duniani, Afrika na hapa nchini. Vinginevyo, sekta hizo zitakosa uhalisia.

### 2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifahamu kwamba, Bunge linapopitisha bajeti ya miradi ya maendeleo linatarajia kuona mabadiliko yanayotokana na utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa utaratibu wa Bunge la Tanzania, ili kujua upatikanaji wa manufaa kutokana na miradi ya Wizara hii, Bunge linategemea Taarifa za Kamati hii. Kwa msingi huo, Kamati hii imefuatilia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu ya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara hii, Kamati ilitembelea miradi minne. Pamoja na ziara hiyo, Kamati ilipokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo. Ufafanuzi zaidi kuhusu Miradi unaambatishwa pamoja na Taarifa hii **(Kiambatisho Na1).** Hata hivyo kwa ujumla Kamati imebaini yafuatayo:

(i) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ni asilimia 57.3 ya bajeti yote.

(ii) Kwa ujumla, upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi minne iliyokaguliwa umefikia wastani wa asiliamia 71.2

(iii) Mwenendo wa Utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, Utekelezaji wa Mradi Na. 6505, Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji wa Magazeti ya Serikali hauendelei kwa kasi iliyokusudiwa.

### 2.2.4 Utekelezaji wa Kazi Zilizopangwa

**Mheshimiwa Spika,** Ili kulijulisha Bunge ufikiaji wa lengo la Bajeti iliyopitishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii, Kamati ilitaka kufahamu tathmini ya hali ya utekelezaji wa kazi zilizopangwa ikilinganmishwa na Bajeti iliyopitishwa na Bunge. Uchambuzi uliofanyika umeonesha kuwa utekelezaji wa mipango na majukumu uliendana na upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, majukumu na mipango ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yanaendelea kutekelezwa vizuri na ufanisi wake unaonekana. Kwa mfano, Wizara ilikuwa imepanga kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997. Taarifa za utekelezaji zimeonesha kwamba, Wizara imeomba ufadhili kutoka ubalozi wa Uswisi na Umoja wa Ulaya ambao kwa pamoja watatoa kiasi cha **Euro 150,000** ili kufanikisha utekelezaji wa jukumu hili. Hatua hii ni mwenendo mzuri wa utekelezaji ingawa bado mchakato unaendelea.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilidadisi zaidi kuhusu mpango wa kuratibu matamasha manne (4) ya kitaifa na kimataifa. Taarifa

zilizowasilishwa kwenye Kamati zilionesha kuwa, Serikali imeendelea na maandalizi ya Tamasha kubwa la ***Samia Serengeti Music Festival*** ikiwa ni mwendelezo wa Tamasha la ***Serengeti Music Festival***. Tamasha hili limekuwa likiendeshwa tangu mwaka 2020 na kufanyika Jijini Dar es Salaam, Bagamoyo na Dodoma.

### 2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** kama alivyosema mtoa hoja, kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 285,318,387,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Uchambuzi ulibainisha yafuatayo:-

(i) Asilimia 9.5 ya Bajeti yote ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ililenga matumizi ya kawaida, Lakini kiasi cha asilimia 14.6 ya fedha yote iliyopatikana kilihusu matumizi ya kawaida;

(ii) Asilimia 58.4 ya bajeti ya matumizi ya kawaida ililenga matumizi mengineyo. Lakini, kiasi cha fedha iliyopatikana kwa ajili ya matumizi mengineyo ni asilimia 68.5 ya fedha iliyopatikana kwa ajili kugharimia matumizi ya kawaida.

(iii) Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,847,483,000.** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 11,280,116,000.** Kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 258,190,788,000**. kwa ajili ya miradi ya maendeleo.


**Mheshimiwa Spika,** Mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na.2**

**Jedwali Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| Maelezo | | Kiasi Kilichoidhinishwa Mwaka 2024/25 | Kiasi Kilichoidhinishwa Baada ya Uhamisho Mwaka 2024/2025 | Kiasi Kilichopokelewa hadi Februari, 2025 | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| Mishahara ya Watumishi | Wizara | 3,989,923,000.00 | 4,345,802,000.00 | 2,547,758,160.73 | 59% |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 7,290,193,000.00 | 18,617,694,014.67 | 5,545,342,076.00 | 30% |
| **Jumla Ndogo** | | **11,280,116,000.00** | **22,963,496,014.67** | **8,093,100,236.73** | **35%** |
| | | | | | |
| | Wizara | 11,263,816,000.00 | 12,801,937,479.00 | 7,811,462,419.47 | 61% |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 4,583,667,000.00 | 13,397,737,665.71 | 9,769,000,180.15 | 73% |
| **Jumla Ndogo** | | **15,847,483,000.00** | **26,199,675,144.71** | **17,580,462,599.61** | **67%** |
| | | | | | |
| Miradi ya Maendeleo | Wizara | 230,685,693,100.00 | 226,375,136,570.49 | 127,315,146,997.76 | 56% |
| | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 27,505,094,900.00 | 35,982,813,777.87 | 23,099,084,202.68 | 64% |
| **Jumla Ndogo** | | **258,190,788,000.00** | **262,357,950,348.36** | **150,414,231,200.44** | **57%** |
| **JUMLA KUU** | | **285,318,387,000.00** | **311,521,121,507.74** | **176,087,794,036.78** | **57%** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Chati Na. 2: Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026*

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya ukusanyaji wa Maduhuli;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya gharama ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; na

(iii) Makadirio ya Matumizi ya Kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia Majukumu ya Msingi ya Wizara hii pamoja na mwelekeo wa Jumla wa Taifa letu. Ulinganisho wa aina za Matumizi ulifanyika kwa kulinganisha na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kwamba, jumla ya **Shilingi 41,331,192,000** zinakadiriwa kukusanywa chini **Fungu 96** kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Maelezo hayo yaliifanya Kamati ilinganishe lengo hilo na lengo lililokuwa limewekwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchanganuzi wa makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 3** na **Chati Na. 3**.


**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2024/2025 na Mwaka 2025/2026**

| Wizara | Makadirio ya Maduhuli 2024/25 | Makadirio ya Maduhuli 2025/26 |
|---|---:|---:|
| Vitambulisho vya Waandishi wa Habari | 30,000,000 | 30,000,000 |
| Machapisho ya picha, mabango na majarida | 50,000,000 | 50,000,000 |
| Usajili wa Magazeti | 50,000,000 | 50,000,000 |
| Ada ya mwaka ya Magazeti | 100,000,000 | 20,000,000 |
| Mapato ya Viwanja vya Michezo (Uhuru, Benjamin Mkapa na Uwanja wa Ndani wa Benjamin Mkapa) | 907,696,000 | 780,795,000 |
| Ada za Mafunzo | 92,302,000 | 105,200,000 |
| Ukumbi wa Mikutano | 1,000 | 1,000 |
| Mapato kutoka vyanzo mbalimbali | 2,000 | 2,000 |
| Marejesho ya fedha za Umma | 2,000 | 2,000 |

| Wizara | Makadirio ya Maduhuli 2024/25 | Makadirio ya Maduhuli 2025/26 |
|---|---|---|
| **Jumla Wizara** | **1,430,003,000** | **1,036,000,000** |
| Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) | 581,700,000 | 1,210,000,000 |
| Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) | 885,000,000 | 1,001,000,000 |
| Bodi ya Filamu Tanzania | 1,460,000,000 | 1,460,000,000 |
| Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) | 1,514,900,000 | 1,653,390,000 |
| Baraza la Michezo la Taifa (BMT) | 1,200,000,000 | 1,200,000,000 |
| Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) | 1,360,000,000 | 1,420,000,000 |
| Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) | 14,685,811,000 | 15,778,540,000 |
| Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) | 16,572,262,000 | 16,572,262,000 |
| **Jumla Taasisi** | **38,259,673,000** | **40,295,192,000** |
| **Jumla Kuu (Wizra + Taasisi)** | **39,689,676,000** | **41,331,192,000** |

**Chanzo:** *Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Chati Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2024/2025 na mwaka 2025/2026**




**Chanzo:** Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makadirio hayo umeonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya makusanyo chini ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026, yameongezeka kwa **asilimia 4** ikilinganiishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Makadirio ya Makusanyo kwa Wizara pekee yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yamepungua kwa **asilimia 28** ikilinganishwa na makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Makadirio ya Makusanyo kwa taasisi zilizochini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa **asilmia 5.3** ikilinganishwa na makadirio hayo kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

**Mheshimiwa Spika**, matokeo hayo yalifanyiwa ulinganisho na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa lengo la kuzingatia uzoefu uliopatikana. Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Ongezeko la **asilimia 4** katika makadirio ya mapato haliendani na uzoefu unaojitokeza katika Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa uzoefu uliopita, hadi kufikia zaidi ya

nusu ya kipindi cha utekelezaji, ukusanyaji ulifika asilima 50, jambo lililoashiria kuwa lengo halina mwelekeo wa kutimia. Hali hii ilionesha kwamba lengo linalowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 linastahili kupungua badala ya kuongezeka.

(ii) Ongezeko la **asilimia 5.3** katika makadirio ya mapato kwa taasisi zilizochini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, limeendana na uzoefu uliopatikana wakati wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, ukusanyaji wa mapato ya taasisi ulifikia asilimia 40 ya lengo, kiwango ambacho kinaashiria kumudu ongezeko la makadirio linalopendekezwa.

(iii) Uwiano wa makadirio ya mapato kati ya wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026, umeendana na uzoefu wa uwiano uliopatikana wakati wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025. Taarifa ya utekelezaji ilionesha kuwa katika ukusanyaji, Taasisi zilikusanya **asilimia 40** ya makusanyo yote na wizara ilikusanya **asilimia 38** ya makusanyo yote. Makadirio kwa mwaka 2025/2026 yanaonesha kuwa makadirio ya mapato ya taasisi ni **asilimia 97** ya jumla ya makadirio yote kwa Fungu 96.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, Wizara imejitahidi kuzingatia uzoefu wa ukusanyaji wa mapato uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Umakini huo wa wizara unahitaji kujitokeza katika maeneo mengine.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 458,190,788,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi huo umefanyika kwa ulinganisho na mwaka wa fedha wa 2024/2025. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kama ifuatavyo:-

(i) Makadirio ya bajeti hii ya miradi ya maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 77.5.**

(ii) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo limechangiwa na mpango wa ujenzi wa viwanja viwili vya Michezo jijini Arusha na Dodoma vinavyoombewa kiasi cha **Shilingi 333,096,682,000.00.**

(iii) Makadirio ya bajeti ya ujenzi wa viwanja viwili vya michezo jijini Dodoma na Arusha ni sawa na **asilimia 72.7** ya bajeti yote ya maendeleo kwa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya Michezo jijini Dodoma na Arusha. Viwanja hivyo,

kwa kiasi kikubwa vitasaidia kuwa na miundombinu bora ya michezo Tanzania.


**Mheshimiwa Spika,** zaidi ya uchambuzi huo, Kamati imefanya ulinganisho wa Bajeti ya miradi ya maendeleo chini ya Wizara hii kwa kulinganisha na Bajeti kuu kwa ajili ya miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026. Uchambuzi huo unaonekana katika **Jedwali Na. 4 na Chati Na. 4**

**Jedwali Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| MLINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **BAJETI** | **BAJETI YA TAIFA 2024/2025 (000,000)** | **BAJETI YA TAIFA 2025/2026 (000,000)** | **ONGEZEKO (000,000)** | **% YA ONGEZEKO YA BAJETI YA TAIFA** | **BAJETI YA WIZARA 2025/2026 (000,000)** | **% YA BAJETI YA WIZARA KWENYE BAJETI YA TAIFA 2025/26** |
| PE | 11,767,675.10 | 13,174,240.50 | 1,406,565.40 | **11.95** | 33,403.81 | 0.25 |
| OC | 21,618,648.60 | 24,457,591.50 | 2,838,942.90 | **13.13** | 28,065.47 | 0.11 |
| DEV | 15,959,364.00 | 19,608,418.40 | 3,649,054.40 | **22.86** | 458,190.79 | 2.34 |
| **JUMLA** | **49,345,687.70** | **57,240,250.40** | **7,894,562.70** | **16.00** | **519,660.07** | **0.91** |

**Chanzo:** *Randama ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu Mwelekeo wa Bajeti kwa Mwaka 2025/2026*

**Chati Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**




**Chanzo:** *Usanifu wa Kamati kutoka kwenye Taarifa za Randama ya Wizara kwa Mwaka 2025/2026*

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya bajeti ya kawaida kwa kutumia njia ya ulinganisho. Aina mbili za bajeti ya matumizi zililinganishwa ambapo uzoefu wa mwaka wa fedha 2024/2025 ulitumika. Matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya matumizi ya kawaidia yameongezeka kwa asilimia 82 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Ongezeko la Bajeti ya mishahara kwa Wizara hii limeongezeka kwa asilimia 196.1 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Bajeti ya matumizi ya uendeshaji yaani matumizi mengineyo imeongezeka kwa asilimia 77.1 Ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(iv) Bajeti ya matumizi mengineyo kwa mwaka 2024/2025 ni sawa na asilima 5.6 ya jumla ya bajeti ya wizara hii. Uwiano huo unatofautiana na mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo bajeti ya matumizi mengineyo ni asilimia 5.4 ya jumla ya bajeti ya wizara.

### 2.4 Majumuisho ya Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii imefafanua mambo makuu mawili: Kwanza ni kuhusu uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na pili ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika sehemu ya kwanza, maelezo yametolewa kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, uchambuzi wa mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa majukumu na mipango ya wizara hii.

**Mheshimwa Spika,** vilevile, sehemu hii imefafanua kuhusu uchambuzi wa makadirio ya maduhuli, uchambuzi wa

makadirio ya bajeti ya miradi ya maendeleo na uchambuzi wa makadirio ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Maelezo yaliyotolewa yameonesha kuwa sehemu ya ushauri uliotolewa unaendelea kufanyiwa kazi, uzoefu wa mwaka wa fedha 2024/2025 umezingatiwa katika bajeti kwa mwaka 2025/2026 na upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge umeendana na majukumu yaliyopangwa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI, USHAURI NA HITIMISHO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokupatikana kwa fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni jambo linaloweza kuathiri matarajio ya miradi iliyopangwa;

(ii) Kukosekana kwa mikakati ya kuboresha viwanja vya michezo nchini, kunafifisha uwezekano wa kuwa na viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa, hali inayoongeza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa (*Benjamini Mkapa Stadium)*.

(iii) Kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ni jambo linaloweza kufanikisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

(iv) Wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali unahitaji kuboreshwa na kuongezwa;

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zipatikane kwa wakati, ili kutozuia ukamilikaji wa mradi wa ujenzi na ununuzi wa mitambo;

(vi) Upo umuhimu wa kufanyika kwa tathmini, uchunguzi na utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utendaji kazi wa TSN.

### 3.3 Ushauri

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na maoni yalivyoelezwa hapo juu, Kamati ilizingatia ipasavyo maoni hayo na kuyatumia kama msingi wa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati na kwa kiwango kilichokusudiwa ili kukidhi matarajio kwa Wizara hii.

(ii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iandae mikakati ya kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya kitaifa na kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamini Mkapa *(Benjamini Mkapa Stadium)*.

(iii) Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Uwanja wa Arusha ili kufanikisha na kukamilisha utekelezaji wa mradi huu kama ilivyokusudiwa na pia kuongeza chachu ya utalii na kuwa kituo muhimu katika Mashindano ya Mataifa ya Afrika (AFCON).

(iv) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo iboreshe na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Mapato ya Tozo za Hakimiliki kwa kuongeza vifaa vinavyotozwa Tozo hii hasa vya Kidijitali.

(v) Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ujenzi na ununuzi wa mitambo ya uchapaji zitolewe kabla ya tarehe 01 Julai, 2025;

(vi) Serikali ifanye tathmini, utafiti kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu utendaji kazi wa TSN ili kuweza kujua ni sababu zipi? zimesababisha jengo la kiwanda cha uchapaji kutokukamilika kwa wakati.

(vii) Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ikamilishe ujenzi wa Jengo la Kiwanda cha Uchapaji ili kupunguza gharama za uendeshaji na utunzaji wa mitambo katika maghala ya Taasisi nyingine.

### 3.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo orodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard):*-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Musa Ramadhani Sima, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Anastazia James Wambura, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Dr. Thea Ntara, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ester Edwin Maleko, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Hassan Zidadu Kungu, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Kassim Ali Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Mohamed Said Issa, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mwanakhamisi Kassian Said, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Nusrat Shaaban Hanje, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Rose Syprian Tweve, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Tunza Issa Malapo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Yahya Ally Hamis, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru – Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa

na Michezo Mhe. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Naibu Waziri - Mhe. Hamis Mohamed Mwinjuma (Mb), Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndg. Gerson Partinus Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Methusela Ntonda, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Idephonce. Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili lijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.



Husna Juma Sekiboko, Mb

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**

**YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**

07 Mei, 2025

## VIAMBATISHO

### KIAMBATISHO NA 1

### YATOKANAYO NA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara za ukaguzi wa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa miradi na kuona hali halisi kwenye maeneo ya utekelezaji wa miradi husika. Uchambuzi wa taarifa hizo ulilinganishwa na hali halisi ya hatua zilizofikiwa pamoja na madhumuni ya kutekelezwa kwa miradi inayohusika. Naomba kutoa taarifa kuhusu matokeo ya ukaguzi na uchambuzi wake kama ifuatavyo:-

**a) Mradi Na. 6586 wa Ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unahusu ujenzi wa Uwanja wa Mpira wa Miguu Jiji la Arusha. Taarifa zinaonyesha kuwa, fedha zinazotumika kutekeleza mradi huu ni fedha za ndani kwa asilimia mia moja, jumla ya **Shilingi 125, 290,774,000** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia Februari, 2025 mradi ulipokea **Shilingi 94,367,727,295.46** sawa na **asilimia 75.3**. Aidha, Kamati imebaini kuwa miongoni mwa kazi zilizofanyika ni kukamilika kwa ujenzi wa msingi wa uwanja (*kitako cha uwanja*) kwa **asilimia 100** na kuanza ujenzi wa

mihimili ya majukwaa na jengo la uwanja kwa **asilimia 36.72**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona ipo tija ya mradi huu kwa kuwa ukikamilika utachukua idadi kubwa ya watazamaji ambapo watu **32,000** wataingia kwa wakati mmoja na utakidhi viwango vya Shirikisho la Mpira wa Miguu (CAF) kwa mashindano husika. Aidha, mradi utawezesha kuongeza chachu ya utalii wa kimichezo katika Jiji la Arusha hivyo kuongeza fursa za ajira kwa vijana wa kitanzania. Kamati imeridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu kwani hadi wakati wa ziara ya Kamati ilikuwa imebaki takribani miezi kumi na nane kufika mwezi Julai, 2026 ambapo mradi unapaswa kuwa umekamilika.

**b) Mradi Na. 4279 Ujenzi wa Makao Makuu ya TBC Vikonje awamu ya kwanza (Lot 1) Dodoma**

**Mheshimiwa Spika;** Mradi huu kwa ujumla wake umekadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi 54,204,499,116.46** kwa awamu ya kwanza. Kamati ilielezwa kuwa, Mradi huu umegawanyika katika sehemu nne:-

**Awamu ya Kwanza ni Ujenzi wa Jengo la Utawala**. Lengo ni kuwa na studio za redio, televisheni na vyombo vya kidijitali. Ujenzi wa awamu ya kwanza utagharimu kiasi cha **Shilingi Shilingi 6,277,718,877.87** ambapo hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha **Shilingi 4,794,780,534.60** kimepokelewa. Jengo hilo linatarajiwa kuwa na Mitambo na miundombinu

yote muhimu ya uandaaji na urushaji wa matangazo (zikiwemo *satellite-uplink*, *transmission studio*, *server based system)*, vitakuwa ni sehemu ya mradi ambapo ukikamilika matangazo yote ya TBC yatarushwa kutokea Dodoma.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilidadisi kuhusu hatua iliyofikiwa ya utekelezaji wa mradi huu na kuelezwa kuwa, mradi wa ujenzi wa Jengo la utawala ulikuwa umefikia **asilimia 48**. Kamati ilibaini kuwa kuna uwezekano mkubwa wa Mradi wa Jengo la Utawala kutokukamilika kwa wakati kwani asilimia za utekelezaji wake hazijafika hata ya nusu ukizingatia umebaki muda wa miezi 7 tu ili kukamilika kwa mradi huo. Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ichukue hatua za makusudi za kuhakikisha fedha zote za mradi huu zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu zinatololewa kabla ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 kukamilika.

**c) Mradi Na. 6523 Ukarabati wa Uwanja wa Uhuru Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ukarabati wa uwanja wa uhuru Dar es Salaam ulitengewa jumla ya **shilingi 4,000,000,000** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2025, jumla ya **shilingi 2,955,015,000.** sawa na **asilimia 73.9** ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina. Aidha, Kamati imebaini kuwa miongoni mwa kazi zilizofanyika ni kuondoa nyasi bandia katika eneo la kuchezea, kutoa rangi ya zamani, mkandarasi ameanza kufunga nguzo za chuma

kwa ajili ya kutoa mabati ya zamani na kuweka mabati mapya na kuandaa sehemu zitakafungwa viti vya watazamaji wakati wa matukio mbalimbali yakiwa yanaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kimsingi ukarabati katika Uwanja wa Uhuru bado upo katika hatua za awali, pamoja na kwamba Mkandarasi amelipwa malipo ya awali (*advance payment*) tangu tarehe 27 Septemba, 2024. Kamati haijaridhishwa na mwenendo wa ukarabati wa uwanja huu kwani kuna changamoto kubwa ambazo zinaweza kusababisha ucheleweshaji wa ukarabati na hata kushindwa kukamilika kwa wakati kutokana na mkandarasi kutekeleza shughuli hii kwa kusuasua na hivyo kuathiri shughuli za uwanja.

**Mheshimiwa Spika,** ukarabati wa uwanja huu ni muhimu sana kwa sababu ni miongoni mwa viwanja ambavyo vitatumika kwa mazoezi katika michezo ya CHAN na AFCON 2027. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha mkandarasi anamaliza kazi kwa wakati ili kuruhusu michezo hiyo kufanyika katika uwanja huu kama ilivyokusudiwa. Aidha, Serikali ihakikishe inatumia wakandarasi ambao wanaendana na kasi ya utekelezaji wa miradi ili kuepusha ucheleweshaji ambao kimsingi hauna tija.

d) **Mradi Na. 6505, Ujenzi na Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji wa Magazeti ya Serikali**

**Mheshimiwa Spika;** Mradi huu kwa ujumla wake umekadiriwa kugharimu jumla ya **Shilingi Bilioni 32.1** hadi kukamilika kwake. Kamati ilielezwa kuwa, ujenzi wa Jengo la kusimika mitambo ya uchapaji na ununuzi wa mitambo ya uchapishaji lengo ni kupunguza gharama za uchapishaji kwa TSN kwenye makampuni binafsi, kupunguza kutegemea ruzuku ya uwekezaji kutoka Serikalini na kulinda usalama wa nyaraka na taarifa muhimu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika;** Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 mradi huu uliidhinishiwa Bajeti ya maendeleo kiasi cha **Shilingi 9,200,000,000.00** ikijumuisha ujenzi wa jengo la kusimika mitambo ya uchapishaji na ununuzi wa mitambo ya uchapishaji. kiasi cha **Shilingi 7,200,000,000** ni kwa ajili ya ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapishaji na **Shilingi 2,000,000,000** ni kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha uchapishaji. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kiasi cha **Shilingi 5,769,821,844.91** kilichotengwa kilikuwa kimepokelewa na mradi umefikia **asilimia 53**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa kuna uwezekano wa kuharibika kwa mitambo iliyohifadhiwa ghalani na iliyopo bandarini, kuhatarisha uhai na ufanisi wa mitambo husika kwani inahitaji mazingira maalumu ya uhifadhi pamoja na kuongezeka kwa gharama za mradi kutokana na kuchelewa kwa fedha kwa ajili ya malipo ya mzabuni na wakandarasi ikilinganisha na matakwa ya kimkataba yanayosababisha mapitio madogo (variations). Ni rai ya Kamati kuwa Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge lako tukufu zitolewe zote na kwa wakati ili mradi huu uanze kufanya kazi na kuleta tija kwa Taifa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na TSN iweke mkakati madhubuti wa kufuatilia fedha kutoka Hazina ili kukomboa mitambo yote iliyokwama bandarini na kuharakisha ujenzi wa kiwanda ili mitambo iliyotunzwa katika maghala ya kukodi iweze kuondolewa.

**KIAMBATISHO NA 2**

## UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO

Wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambapo maelezo ya Wizara kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri huo ni kama ifuatavyo:-

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | BAKITA iweke mikakati ya makusudi ya kubidhaisha lugha ya Kiswahili kwa kuzalisha Wakalimani wengi zaidi ambao watakuwa na uwezo wa kufahamu lugha zaidi ya moja kwa ufasaha ikiwa ni pamoja na kuongeza nyenzo muhimu za kufundishia. | Wizara kupitia BAKITA imeendelea kuimarisha wakalimani wa lugha mbalimbali kwa kutoa mafunzo kwa wakalimani 176 wa lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu, Kihispaniola, Kijerumani na Kichina ambapo kutoka Kishwahili – Kiingereza wakalimani 100; Kiswahili – Kiingereza – Kifaransa 30; Kiswahili – Kiingereza – Kiarabu 19; Kiswahili – Kiingereza – Kireno 9; Kiswahili – Kiingereza – Kichina 7; Kihispaniola – Kiingereza 2; Kifaransa – Kihispaniola 1; Kiswahili – Kituruki 1; Kiingereza – Kijerumani 1; Kifaransa – Kiarabu 1; Kiingereza – Kirusi 3; Kiingereza – Kiitaliano 1; na Kiamharik – Kiswahili 1. Aidha, BAKITA imeendelea na uandishi wa vitabu mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia ikiwamo Mwongozo wa Kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni, Mwongozo wa kutahini Kiswahili kama lugha ya kigeni na kutoa toleo la pili la kitabu cha kufundishia, cha Furahia Kiswahili. Vilevile, BAKITA imeandaa nyenzo |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | za kiteknolojia ili kurahisisha upelekaji wa lugha kimataifa. |
| 2. | Ili kufanikisha kubidhaisha Kiswahili, Serikali ianzishe Dawati la Kiswahili katika kila Ubalozi kama wenzetu China wanavyofanya. Aidha, katika kuimarisha matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa waandishi wa Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Kamati inasisitiza kuwa, Wizara itumie Balozi zetu kujenga ushawishi wa Vyuo Vikuu vya nje ya nchi pamoja na Taasisi zingine kufundisha Kiswahili kama somo katika vyuo na Taasisi hizo. | Katika kutekeleza hili, Serikali imeanza na balozi 10 kwa kufungua madawati ya Kiswahili kufundisha lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Balozi hizo ni<br><br>Ufaransa, Uholanzi, Italia, Jamhuri ya Korea, Nigeria, Zimbabwe, Umoja wa Falme za Kiarabu, Mauritius, Sudani na Msumbiji. Pia, balozi za Ujerumani, Namibia na Afrika Kusini zimefungua maktaba za vitabu vya Kiswahili kama moja ya njia ya kutangaza Kiswahili katika maeneo hayo.<br><br>Aidha, baadhi ya balozi zimefanya ushawishi kwa vyuo vikuu na taasisi mbalimbali kufundisha Kiswahili mathalani ubalozi wa Nigeria umefanya ushawishi katika Chuo Kikuu cha Port Hacourt kufundisha Kiswahili na tayari wamesaini Hati ya Makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Halikadhalika, balozi za Tanzania nchini Zambia na Msumbiji zimejenga ushawishi na vyuo vikuu vya Taifa vya nchi hizo na tayari wameridhia ufundishaji wa Kiswahili. Vilevile, ubalozi wa Ethiopia umefanya ushawishi kwa Chuo Kikuu cha Ethiopia na tayari wamefanya mazungumzo na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya kuanza kufundisha Kiswahili. Pia, Chuo Kikuu cha Juba- Sudani Kusini kimeingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanza kufundisha Kiswahili na hati ya makubaliano tayari imesainiwa.<br><br>Vyuo vikuu vingine vilivyoshawishiwa na |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | tayari vimeanza kufundisha Kiswahili ni Chuo kikuu cha Komoro walioingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar – SUZA, Chuo Kikuu cha Cape Town cha Afrika Kusini ambacho kimeanza kufundisha Kiswahili baada ya kusaini hati ya makubaliano na Chuo Kikuuu cha Dar es Salaam. Pia, Chuo Kikuu cha Havana nacho kimeanza kufundisha Kiswahili baada ya kuingia makubaliano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Fauka ya hayo, kwa sasa ubalozi wa Komoro umejenga ushawishi wa kuingiza Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini humo na tayari wameridhia.<br><br>Balozi wa Tanzania nchini Msumbiji ambaye anasimamia nchi za Eswatini na Madagascar anaendelea na mazungumzo ya kuingiza Kiswahili katika mfumo wa elimu wa Eswatini. Aidha, vyuo vikuu vingine barani Afrika ikiwemo Zimbabwe na Ghana, Rwanda, Burundi navyo vinafundisha Kiswahili. |
| 3. | Serikali iongeze bajeti ya BAKITA ili kuongeza kasi ya kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi. | Serikali inatambua umuhimu wa BAKITA katika kuendeleza lugha adhimu ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha pekee iliyozaliwa Afrika ambayo ni mali ya Waafrika. Kwa kutambua hilo Serikali imeendelea kuimarisha bajeti ya BAKITA. Kwa mwaka 2024/25 BAKITA ilitengewa bajeti ya maendeleo jumla ya shilingi milioni 500 ikilinganishwa na mwaka 2023/24 ambapo ilitengewa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kutekeleza Mkakati wa Taifa wa kupeleka Kiswahili kimataifa. Pamoja na kutengewa bajeti ya Shilingi milioni 500, Baraza likiwa katika utekelezaji wa majukumu yake, Serikali ililazimika kuliongezea bajeti ya |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | kiasi cha Shilingi<br><br>1,591,164,900 kwa ajili ya kuwezesha kongamano la kwanza la Kimataifa lililofanyika jijini Havana Cuba ikiwa ni mkakati wa makusudi wa kupeleka Kiswahili kwa mara ya kwanza katika ukanda wa nchi zenye wazungumzaji wa Kihispaniola katika ukanda wa Karibe na Amerika Kusini. Katika mwaka 2025/26, BAKITA imetengewa Shilingi 3,400,000,000 kwa ajili ya shughuli za ubidhaishaji wa Kiswahili. |
| 4. | Serikali ihakikishe inasimamia vizuri matumizi ya fedha za Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili ziweze kuleta tija ya kweli kama ilivyokusudiwa na Mheshimiwa Rais katika azma yake ya kuendeleza Wasanii. | Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania unafanya kazi kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB na NBC. Dhumuni la ushirikiano huu ni kutumia utaalamu wa benki katika kuchakata mikopo, ufuatiliaji wa maendeleo ya miradi na marejesho pamoja na kutoa ushauri wa kibiashara katika miradi inayoombewa mikopo. Mfuko umejikita katika utoaji wa elimu ya usimamizi wa miradi, biashara na fedha kabla ya Msanii kupata mkopo na baada ya mkopo, ili kuhakikisha kuwa fedha zinatumika ipasavyo na miradi inakuwa na tija katika jamii. Aidha, Mfuko umeshawajengea uwezo jumla ya wanufaika (wadau ambao mikopo yao imepitishwa)<br>232. Kati ya wanufaika hao, Sanaa za Ufundi ni 88, Muziki 49, Maonesho 54, Lugha na Fasihi 9, na Filamu 32. Kutokana na uwezeshaji huo kiwango cha marejesho kimeongezeka kutoka asilimia 89 hadi asilimia 96. |
| 5. | Serikali iweke mikakati ya | Serikali inafanya kila juhudi kuongeza bajeti ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | kuongeza fedha kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili uweze kuwafikia walengwa wengi zaidi na ibuni vyanzo vingine vya kutunisha Mfuko. | kwa lengo la kuongeza ukopeshaji kwa wasanii. Kupitia bajeti ya maendeleo Serikali iliongeza bajeti ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kutoka shilingi bilioni 1.6 kwa mwaka wa fedha 2023/24 hadi shilingi Bilioni 3 kwa mwaka wa fedha 2024/25. Hivyo, kiasi cha fedha kilichoongezeka ni shilingi bilioni 1.4, sawa na asilimia 87.5. Serikali imechukua jitihada mbalimbali za kuongeza vyanzo vingine vya mapato ikiwemo Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kupokea asilimia 10 ya makusanyo yanayotokana na tozo ya hakimiliki (Copyright Levy) kwenye vibebeo vya kazi za sanaa na ubunifu. Katika mwaka 2025/26, Serikali imeendelea kuongeza bajeti ya Mfuko hadi kufikia shilingi bilioni 4 kwa ajili ya utoaji wa mikopo, ruzuku na mafunzo kwa wadau wa utamaduni na sanaa. Kutokana na kuongezeka kwa bajeti kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Februari, 2025, Serikali kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umetekeleza utoaji wa mikopo ifuatavyo:<br><br>(a) Kuwezesha utoaji mikopo yenye thamani ya Shilingi 2,692,217,069.89 kwa miradi 143 ya Utamaduni na Sanaa katika mikoa 9 nchini ambayo ni Ruvuma, Geita, Mara, Arusha, Morogoro, Pwani, Mwanza, Mbeya na Dar es Salaam;<br>(b) Utoaji mikopo kisekta: Sekta zilizonufaika ni Filamu miradi 37 shilingi 645,130,090; Ufundi miradi 59 shilingi 997,129,629.89; Maonesho miradi 19<br>shilingi 349, 988,000; na Muziki miradi 23 shilingi 592,280,750; na<br>(c) Utoaji mikopo kimakundi: Makampuni |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | 13 yamewezeshwa Shilingi 444,747,000; vikundi vya Bendi 17 Shilingi 325,870,000; waombaji binafsi<br>Wanawake 48 waliwezeshwa Shilingi 715,600,000 na wanaume 65waliwezeshwa Shilingi 1,206,000,069.89. |
| 6. | Serikali iimarishe uratibu na usimamizi wa Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania katika eneo la ukusanyaji wa fedha za marejesho ya mikopo ili kuwapa fursa wasanii wengine waweze kupata mikopo na kuimarisha ukuaji wa sekta za utamaduni na sanaa. | Wizara iliingia makubaliano na Mkusanya Madeni *(debts collector)* Mchinga Auction Mart and Real Agency Company Limited tarehe 12 Agosti, 2024 kwa ajili ya kukusanya madeni ya wadaiwa sugu waliowezeshwa na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kabla ya kuingia katika ushirikiano na Taasisi za Fedha. Aidha, hadi kufikia mwezi Februari, 2025, kiasi cha Shilingi 68,265,875 kimekusanywa kati ya Shilingi 363,789,395 zilizokuwa zinadaiwa. Wizara inaendelea kumsimamia Mkusanya Madeni ili akamilishe jukumu lake kulingana na mkataba uliosainiwa. |
| 7. | Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania yenye maudhui ya kulinda Mfuko | Wizara imeshaandaa rasimu ya andiko la Sheria ambapo kwa sasa lipo katika hatua ya kulipitisha kwa wadau kwa ajili ya maoni. Aidha, andiko linatarajiwa kukamilika na kuanza hatua za uidhinishaji Serikalini ifikapo mwisho wa Machi, 2025. |
| 8. | Serikali itoe mafunzo kwa walengwa kuhusu matumizi ya mikopo au ruzuku zitakazotolewa na Mfuko kwa namna iliyokusudiwa yenye kuleta tija kwao na katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa. | Mfuko kwa kushirikiana na wadau umewajengea uwezo wasanii 3,895 wakiwemo wanawake 2,306 (asilimia 59.2) na wanaume 1,589 (asilimia 40.8) kutoka mikoa sita<br>(6) ambayo ni Ruvuma, Pwani, Dar es Salaam, Katavi, Singida na Shinyanga.<br><br>Mafunzo kwa walengwa, yalijumuisha mada mbalimbali kama vile usimamizi wa miradi, |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | uwekaji akiba, umuhimu wa urasimishaji, uandishi wa maandiko ya miradi, urasimishaji wa Sanaa, Sanaa na afya, biashara na familia na uwekaji wa kumbukumbu wa mapato na matumizi ya kila siku. |
| 9. | Fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa zipatikane kwa wakati. | Uwanja wa Benjamin Mkapa, ni miongoni mwa viwanja ambavyo vitatumika katika michezo ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Uwanja huu unafanyiwa ukarabati mkubwa kwa gharama ya Shilingi 31,329,180,963.16 ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Katika mwaka 2024/25, Uwanja ulitengewa jumla ya Shilingi 26,629,220,000. Wizara inashirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zilizotengwa kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa zinapatikana na mkandarasi analipwa kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba ambayo ni kwa utaratibu wa hati za malipo (Certificate of Payment). Hadi mwezi Februari, 2025 jumla ya hati za malipo tano (5) zimepokelewa kutoka kwa Mshauri Elekezi. Serikali imefanya malipo ya hati zote tano, ambayo ni jumla ya Shilingi 13,555,981,449.85. Hivyo, Mkandarasi amelipwa hati zote alizoziwasilisha Serikalini kwa ajili ya malipo, hakuna hati ambayo inadaiwa. Aidha, kazi ya ukarabati inaendelea, hadi kufikia mwezi Februari, 2025 kazi imefikia asilimia 80. Hatua iliyobaki ni ufungaji wa viti vya uwanja mzima takribani viti 62,000 ambapo viti 40,000 vimekwisha wasili na kazi ya ufungaji imekwisha anza, kurudishia mifumo ya TEHAMA, kufunga viyoyozi na upakaji wa rangi kwenye baadhi ya vyumba ili kufikia |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | | asilimia 100 ya utekelezaji. |
| 10. | Serikali iandae mkakati wa kuboresha viwanja vingine vyenye hadhi ya kuendesha mashindano ya Kimataifa ili kupunguza mfululizo wa matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa. | Uwanja wa Benjamin Mkapa ni uwanja pekee Tanzania wenye viwango vya FIFA. Uwanja huu umekuwa na matumizi mengi kutokana na kukosekana kwa mbadala wake.<br><br>Hata hivyo, Serikali imechukuwa juhudi za makusudi za kuhamasisha Serikali za Mitaa na sekta binafsi kujenga viwanja ili kupunguza kutumika kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa. Baadhi yao walioitikia wito huo na kujenga viwanja hivyo, ni Azam Complex – Chamazi, Gwambina – Misungwi, KMC – Kinondoni, Majaliwa Complex – Ruangwa, Singida Black Stars - Singida, Black Rhino-Karatu n.k. ambapo kutokana<br><br>na kuwepo kwa viwanja hivyo kumesaidia kupunguza matumizi ya Uwanja wa Benjamin Mkapa.<br><br>Tatizo la kutumika kwa Uwanja wa Benjamin Mkapa litakwisha kabisa baada ya kukamilika kwa ukarabati wa Uwanja wa Uhuru, Gymkhana, Mej Gen. Isamuhyo, Farasi, Leaders Club, Shule ya Sheria (Law Schools of Tanzania), TIRDO, na kukamilika kwa ujenzi wa viwanja vya Arusha na Dodoma. |
| 11. | Menejimenti ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ihakikishe inafanya ukarabati wa uwanja mara kwa mara kadri inavyohitajika ili kuepuka gharama kubwa | Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa muda mrefu haujafanyiwa ukarabati kutokana na kukosekana kwa fedha za kufanya hivyo. Uwanja huu umeanza kutumika mwaka 2007. Tangu uanze kutumika uwanja huu, haukuwahi kufanyika ukarabati mkubwa kama unaoendelea. Ukarabati |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | zisizo za lazima. | unaoendelea umeanza kufanyika mwaka 2023 takribani miaka 16 tangu uanze kutumika. Kwa sasa Serikali inaendelea na ukarabati ili kuweza kuurejesha katika hali yake ili uweze kutumika katika michezo mikubwa ijayo ya CHAN 2024 na AFCON 2027. Baada ya ukarabati huo kukamilika, Serikali itahakikisha uwanja huu pamoja na viwanja vingine vinavyojengwa katika miji ya Arusha na Dodoma havitakaa kwa muda mrefu bila ya kukarabatiwa. Hili litawezekana tu kwa kuwa Serikali ipo katika mpango wa kuanzisha Taasisi maalumu itakayohusika na usimamizi wa miundombinu ya michezo nchini, ikiwemo viwanja vyote vya mpira wa miguu vinavyomilikiwa na Serikali ambavyo vinatarajiwa kuongezeka baada ya michezo ya CHAN 2024 na AFCON 2027.<br><br>Kutokana na kuanzishwa kwa Taasisi hiyo, ni imani ya Serikali kuwa makusanyo yanayotokana na shughuli za michezo katika viwanja hivyo yatabaki katika viwanja husika kwa ajili ya ukarabati wa kila siku na shughuli nyingine zinazohusiana na kiwanja husika, badala ya kuyapeleka mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama inavyofanyika kwa sasa. |
| 12. | Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha Mkandarasi wa Uwanja wa Benjamin Mkapa anamaliza kazi kwa wakati ili kuruhusu michezo iliyozuiliwa kuendelea katika Uwanja | Serikali inafuatilia kwa karibu ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati. Ukarabati wa uwanja huu ni lazima ukamilike kwa wakati kwa sababu ni miongoni mwa viwanja vinavyotegemewa kutumika katika<br><br>michezo mikubwa ijayo ya CHAN 2024 na |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | huo. | AFCON 2027. Ukarabati unaendelea vizuri hadi mwezi Februari, 2025 umefikia asilimia 80. Changamoto inayosababisha uwanja huu kushindwa kukamilika kwa wakati ni kuwa uwanja pekee ambao unakidhi vigezo vyote vya FIFA, hivyo wadau kuendelea kufanyia michezo yao katika uwanja wakati wa ukarabati.<br><br>Serikali kupitia Mshauri Elekezi inamsimamia Mkandarasi kwa ukaribu ili aweze kumaliza kazi kwa wakati kutokana na mkataba wa utekelezaji uliopo. Aidha, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini cha Wizara nacho kinaendelea kufuatilia utekelezaji kulingana na ratiba ya maboresho iliyowasilishwa na Mkandarasi kwa Mshauri Elekezi ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). |
| 13. | Serikali ifanye tathmini na ufuatiliaji wa kina kuhusu utendaji kazi wa mkandarasi anayekarabati Uwanja wa Benjamin Mkapa (BECG) kama anastahili kuendelea na kazi. | Wizara kupita Mshauri Elekezi (TBA) inamfuatilia na kumsimamia kwa ukaribu Mkandarasi Beijing Construction Engineering Group Company Limited (BCEG) kuhakikisha anafanya kazi kwa viwango na ubora unaotakiwa kulingana na mkataba wa kazi na kukamilisha mradi kwa kuzingatia makubaliano ya kimkataba. Pamoja na changamoto zilizopo, baada ya Serikali kukaa na Mshauri Elekezi na kushauriana kwa kina Mkandarasi anaendelea kutekeleza majukumu yake. |
| 14. | Serikali itoe fedha zinazotokana na Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Michezo (Sports Betting) kwa wakati kama | Asilimia 5 ya fedha inayotokana na michezo ya kubashiri matokeo ya michezo ipo kisheria na hutumika katika maendeleo ya michezo ikiwemo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo pamoja na |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | ilivyoelezwa na sheria iliyopitishwa na Bunge ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu. | kuwezesha timu mbalimbali kushiriki katika michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Kwa mwaka wa fedha 2024/25, Mfuko wa Maendeleo ya Michezo uliidhinishiwa bajeti ya maendeleo jumla ya kiasi cha Shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya michezo. Hadi kufikia Februari, 2025 Mfuko wa Maendeleo ya Michezo umepokea jumla ya Shilingi 5,617,086,877.51 sawa na asilimia 70 ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha hizi zinatumika kusaidia timu za Taifa na maandalizi ya CHAN 2024. |
| 15. | Serikali izitake Halmashauri zote nchini kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha Programu ya Mtaa kwa Mtaa katika ngazi husika. | Katika kuendesha programu ya Mtaa kwa Mtaa ya kuibua vipaji katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo, Serikali ilitafuta wafadhili ambao walitoa mipira 1,800 na jezi 2,634 ambazo ziligawanywa katika mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kwa ajili ya programu hiyo. Katika hatua nyingine Wizara inawasiliana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kuhakikisha Halmashauri zinatenga fedha kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo katika ngazi ya mitaa nchi nzima. |
| 16. | Serikali iendelee kutenga Bajeti ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo ili kuimarisha michezo, kufadhili timu nyingi zaidi na masuala yote yanayohusu michezo ya kitaifa. | Katika mwaka 2024/25 Serikali imetenga jumla ya kiasi cha Shilingi 8,000,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Maendeleo ya Michezo. Aidha, kiasi cha shilingi 12,000,000,000 kimetengwa katika mwaka 2025/26. |
| 17. | Serikali kupitia BMT iweke mikakati itakayowezesha kuongeza mapato ya Mfuko wa Michezo kutokana na fursa zilizopo ili | Mikakati iliyopo kwa ajili ya kuongeza mapato ya Mfuko ni pamoja na kutumia mapato ya bahati Nasibu ya Taifa kwa ajili ya kuongeza mapato ya Mfuko wa Michezo. BMT inatakiwa kupata asilimia 50 |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | kusaidia shughuli za maendeleo ya michezo. | ya mapato ghafi kutokana na Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Machi 2025, tayari Wizara ya Fedha imeshapata mzabuni kwa ajili ya kuendesha Bahati Nasibu hiyo. Mikakati mingine ni pamoja na kushirikisha wadau wa Michezo, kampuni binafsi, taasisi za fedha, Washirika wa maendeleo na Asasi za Kiraia kwa ajili kuchangia ugharamiaji wa shughuli za michezo, mathalani JICA, ubalozi wa Ufaransa ambao wamekuwa wakichangia shughuli za Michezo. Aidha, Wizara kupitia BMT inaendelea na ujenzi wa kituo cha Mafunzo kwa ajili ya michezo mbalimbali kilichopo katika Mkoa wa Manyara ambacho kitakuwa sehemu ya chanzo cha mapato kwa ajili ya mfuko huu. |
| 18. | Serikali iisaidie TBC ipate fedha za kutosha ili iweze kujiendesha kibiashara sambamba na kuboresha usikivu hasa maeneo ya mipakani na kuboresha miundombinu iliyochakaa. | Katika kuhakikisha kuwa TBC inapata fedha za kutosha, Serikali imeendelea kuiongezea Bajeti TBC kila inapopatikana nafasi ya kufanya hivyo. Bajeti ya TBC ya Matumizi Mengineyo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 4.7 mwaka 2024/25 hadi bilioni 6.19 mwaka 2025/26 na kwa bajeti ya Miradi ya Maendeleo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 9.8 mwaka 2024/25 hadi Shilingi bilioni 14.8 mwaka 2025/26. Ili kuongeza mapato kwa TBC, Serikali imekamilisha mchakato wa kutunga Sheria ya TBC ambayo ilikamilishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Januari, 2025. Sheria hii itasaidia TBC kutafuta na kuanzisha vyanzo vya mapato vya uhakika na vya kudumu. |
| 19. | TBC ifanye maboresho ya miundombinu ya hifadhi za | TBC imekamilisha uchambuzi wa hotuba za viongozi zilizopo katika maktaba zake za redio na televisheni. Jumla ya hotuba 5,000 |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
| --- | --- | --- |
| | hotuba za viongozi ili iwe ya kidijitali na kuwekwa katika majukwaa mbalimbali na mitandao ya kijamii (Mf. YouTube). | zimefanyiwa uchambuzi na tepu 300 zimehamishwa kutoka katika mfumo wa analojia kwenda kidijiti. Aidha, zoezi la kuziwekea utambulisho maalumu (water mark) ili kuziwezesha kupelekwa kwenye majukwaa ya mitandaoni ikiwemo Youtube linaendelea. |
| 20. | Serikali iboreshe posho na stahiki kwa watumishi wa TBC na walipwe kwa wakati ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi. | Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi na kuhakikisha kuwa malipo ya posho na stahili nyingine yanafanyika kwa wakati. Serikali imelipa stahili za madeni ya watumishi kiasi cha Shilingi 3,358,302,001 baada ya madeni hayo kukaguliwa na kuidhinishwa. Mkakati wa kuondokana na changamoto hii ni mchakato wa kutungwa kwa Sheria ya TBC ambao utawezesha kuwepo kwa vyanzo vya uhakika vya mapato. |
| 21. | Serikali iwezeshe TBC kupata mgao wa fedha kutoka kwa wadau wa Safari Channel ili waweze kufanya maboresho ya vipindi na kuchochea utalii. | Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kuwa Taasisi na Wizara wadau wa Utalii wanashiriki katika kuchangia bajeti ya uendeshaji wa Safari Chaneli kila mwaka. Katika kuhakikisha kuwa suala hili linafanikiwa, tarehe 30 Januari, 2025 Bunge lilipitisha Sheria ya TBC ambayo imeainisha vyanzo vya mapato ya uendeshaji wa chaneli za kimkakati ikiwemo chaneli ya Utalii. Aidha, katika kipindi ambacho Sheria haijaanza kutumika wadau wa Chaneli ya Utalii wanaendelea kuchangia bajeti ya uendeshaji. |
| 22. | Serikali iongeze uwezo wa fedha kwa UCSAF ili iweze kuisaidia TBC kuongeza | TBC na UCSAF zimekuwa na ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya upanuzi wa usikivu hasa maeneo ya mipakani. Hadi |

| Na. | Maoni na Ushauri | Utekelezaji |
|---|---|---|
| | usikivu maeneo ya mipakani. | Februari, 2025 miradi ambayo imetekelezwa kwa ushirikiano kati ya TBC na UCSAF imefanyika katika Wilaya 20. |
| 23. | Serikali iisaidie TSN ili waweze kulipwa madeni wanayozidai Taasisi za Serikali. | Hadi kufikia Machi, 2025 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) inazidai Taasisi za Umma jumla ya Shilingi Bilioni 7.3. Kutokana na juhudi zilizofanywa na Kampuni, imefanikiwa kukusanya madeni ya jumla ya shilingi bilioni 1.5. |
| 24. | Kutokana na ununuzi wa mitambo inayoendelea kufanyika katika kampuni ya TSN, Serikali iendelee kuisimamia TSN ili iweze kujiendesha kibiashara. | Katika Mwaka wa Fedha 2024/25 TSN ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni tano (5). Hadi Machi, 2025 fedha zimepokelewa kwa asilimia 100. Aidha, baada ya mapitio ya bajeti ilibainika mahitaji ya kiasi cha shilingi bilioni 4.2. Wizara tayari imepokea jumla ya shilingi 707,567,321 kwa ajili ya malipo ya Hati ya malipo Na. 4 ya Mkandarasi wa ujenzi wa mradi Na. 6505. |
| 25. | Kamati inazishauri Taasisi za Serikali kutumia TSN katika huduma za machapisho, majarida na makala. | TSN kwa kushirikiana na Idara ya Habari-MAELEZO wameendelea kutoa ushawishi kwa Idara, Mashirika na Taasisi za Serikali kuchapisha makala na matanagazo na TSN. Mathalani katika Mkutano wa Kimataifa wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika, TSN ilipata kiasi cha Shilingi 20,000,000 na inatarajia kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia. Matarajio ya TSN ni kwamba utakapokamilika mradi wa ujenzi na usimikaji mitambo ya uchapaji mapato yataongezeka kwa sababu wigo wa biashara utaongezeka. |